

## Maswali

1. Jina la kuhani liliitwa nani?
2. Mkewe aliitwa nani?
3. Walitaka nini?
4. Zakaria aliona nini Hekaluni?
5. Malaika Gabrieli aliambia Zakaria nini?
6. Waliitaje mwanao?
7. Mungu aliambia Yohana afanye nini akiwa mkubwa?
8. Mbona Yohana hakutaka kubatiza Yesu?
9. Mbona Yesu alitaka abatizwe hata kama hakukuwa na dhambi za kuoshwa?
10. Nini ilifanyika baada ya Yesu kubatizwa?

## Majibu

1. Kuhani aliitwa Zakaria.
2. Mkewe aliitwa Elisabeti.
3. Walitaka mtoto.
4. Zakaria aliona malaika Gabrieli Hekaluni.
5. Malaika aliambia Zakaria kwamba watapata mwana.
6. Waliita mwanao Yohana.
7. Mungu aliambia Yohana ambie watu juu ya Ufalme wa Mungu na Mwanawe Yesu Kristo. Aliambia Yohana abatize watu.
8. Kwa sababu hakufanya makosa yoyote. Hakukuwa na dhambi za kuoshwa.
9. Yesu alitaka kutii Mungu na kumpendeza. Alitonyesha mfano.
10. Yesu alipobatizwa, hua ilitoka mbinguni na kutua kwa mabega yake. Sauti kutoka mbinguni ilisema, “Huyu ni Mwanangu mpendwa, ninayependezwa naye.”

# SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 1 Mwaka wa 3



## 38 Yohana anambatiza Yesu

### Marejeo

Mathayo 3:13 – 17

### Kiini cha somo

Kuonyesha vile Yesu alimtii Mungu na vile alionyesha kwamba ubatizo ni wa maana.

### Maneno maalum

- 38.1 Zakaria + Elisabeti + alitaka mtoto + malaika Gabrieli + pata mtoto + Yohana + Zakaria + hakuweza kuzungumza
- 38.2 Mtoto kazaliwa + multe Yohana + Zakaria anazungumza
- 38.3 Yohana akakua + Mungu + ambia watu + Ufalme wa Mungu + batiza + osha dhambi + Mto wa Yordani
- 38.4 Yesu + uliza Yohana + nibatize +hakuna dhambi + heshimu Mungu
- 38.5 Yohana + Yesu + Mto wa Yordani + batizwa + mbingu zikafunguka + hua + Huyu ni Mwanangu mpendwa + Mungu alipendezwa

**38.1** Zakaria alikuwa kuhani na mkewe aliitwa Elisabeti. Zakaria na Elisabeti walitaka mtoto sana lakini hawakupata.

Siku moja Zakaria alikuwa kwa hekalu akiomba. Punde tu aliona malaika amesimama karibu naye. Mwanzoni aliogopa, lakini malaika aliyeitwa Gabrieli, alimwambia asiogope. Gabrieli alimwambia Zakaria kwamba yeye na Elisabeti watapata mtoto atakayeitwa Yohana.

Zakaria alichanganyikiwa, akufurahi tena hakuamini. Malaika alimpa ishara ya kuonyesha kwamba kweli watapata mtoto. Ishara ilikuwa kwamba Zakaria hataweza kuzungumza tena mpaka mtoto atakapozaliwa. Zakaria alienda nyumbani upesi kwa Elisabeti ili amwambia hiyo habari njema.

**38.2** Mwishowe mtoto alizaliwa, vile malaika alikuwa amesema. Kalikuwa katoto kadogo. Marafiki wa Elisabeti walitaka mtoto aitwe Zakaria jina la babaye. Lakini Elisabeti aliwambia kwamba ataitwa Yohana vile malaika alikuwa amesema. Walimpa Zakaria karatasi ili aandike jina lenye alitaka mtoto wake aitwe. Aliandika, "Jina lake ni Yohana." Punde tu, Zakaria alianza kuzungumza. Aliwambia kwamba mtoto lazima aitwe Yohana kwa sababu malaika alimpa lile jina.

**38.3** Yohana alipokua mkubwa, Mungu alimwambia ambie watu juu ya Ufalme wa Mungu na Mwanawe Yesu Kristo. Yohana alikuwa abatize watu, yaani kuwazika ndani ya maji kwa undoleo la dhambi zao.

Siku moja Yohana alikuwa amesimama kando ya Mto wa Yordani akiambia watu vile itakuwa vizuri kwenda kwa Ufalme wa Mungu, wakati kila mtu atakuwa mzuri, wa upendo na furaha na amani.


**38.4** Yohana alikuwa akiambia watu kutubu dhambi zao na wabatizwe. Yohana alibatiza watu kwa Mto wa Yordani.



Yesu alikuja kutoka Galilaya kusikiliza maneno ya Yohana. Yesu aliuliza Yohana ambatize naye pia. Lakini Yohana alitikisa kichwa chake. Yohana alisema, "Ni vyema mimi kubatizwa na wewe kwa sababu wewe hauna dhambi. Haujafanya kosa lolote."

Yesu alimtabasamu na kueleza Yohana, "Mungu anataka nitii amri zake na nibatizwe, kwa hivyo tafadhali nibatize."

**38.5** Kwa hivyo Yohana alichukuwa Yesu mpaka Mto wa Yordani na kumzika ndani ya maji. Yesu alipotoka majini, mbigu zilifunguka na hua ilitoka huko na kutua juu ya mabega ya Yesu. Mungu alimpa Yesu nguvu za kufanya miujiza na sauti ilitoka mbinguni na kusema, "HUYU NI M W A N A N G U M P E N D W A , NINAYEPENDEZWA NAYE."



Mungu alifurahi kwa sababu Yesu alikuwa amebatizwa. Yesu wakati wote alifanya kila kitu kilichopendeza Baba yake. Baada ya ubatizo wake, Yesu alitembea nchi yote ya Israeli akiambia watu juu ya Ufalme wa Mungu wa ajabu utakaosimamishwa hapa duniani. Aliponya wagonjwa na kusaidia wote waliohitaji.